



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 OKTOBA, 2021 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2021.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 OKTOBA, 2021.

Katika dekadhi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini (St. Helena na Mascarene) ilidhoofika kidogo wakati ile iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilionyesha mabadiliko kidogo. Hali hii iliendelea kusababisha upepo wenye nguvu ya wastani kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea maeneo ya pwani ya Bahari ya Hindi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana mashariki mwa bahari ya Hindi wakati magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikuwa la wastani. Hali hii iliendelea kuleta mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kusababisha vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo hayo. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana upande wa kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kupunguza kasi ya upepo uvumao kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu. Hata hivyo, maeneo machache yaliyo karibu na ziwa Tanganyika yalipata vipindi vya mvua na ngurumo kutokana na pepo za Magharibi katika tabaka la chini kuvuma katika maeneo hayo hususani mwishoni mwa dekadhi hii.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 OKTOBA, 2021.

Kwa ujumla, viashiria vya hali ya hewa hapo juu kwa pamoja vilipelekea kusababisha vipindi vya mvua nyepesi pamoja na upepo wa wastani katika maeneo ya pwani ya bahari ya Hindi na vipindi vichache vya mvua na ngurumo katika maeneo ya Magharibi mwa nchi pamoja na mikoa inayozunguka ziwa Viktoria.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2021

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2021

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini (St. Helena na Mascarene) katika dekadhi hii inatarajiwa kudhoofika wakati ile iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuimarika kidogo. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa Mashariki mwa bahari ya Hindi wakati Magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuleta mchango kidogo

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la wastani linatarajiwa upande wa kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na kuwa na mchango kidogo wa kusukuma upepo uvumao kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu. Kwa ujumla, mifumo hii tajwa ya hali ya hewa inatarajiwa kusababisha maeneo ya ukanda wa pwani kuendelea kupata vipindi vya mvua nyepesi wakati Magharibi mwa nchi na maeneo yanayolizunguka ziwa Viktoria yanatarajiwa kuendelea kupata vipindi vichache vya mvua na ngurumo. Maeneo mengine ya nchi yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2021.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vichache vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla na yenye vipindi vichache vya mvua nyepesi.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vifupi vya mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa hususani katika nusu ya kwanza ya dekad.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla na yenye vipindi vichache vya mvua nyepesi.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

727F -00/2019